**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA.**
**S.L.P 54 MUSOMA.**
**SIMU : 0755 671818, 0752525063, 0767 082905.**
**Email:musomatechsecondaryschool@gmail.com**

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA MWAKA 2026.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha **KWANZA** katika Shule hii kwa mwaka **2025**

Shule ya Sekondari **MUSOMA UFUNDI** ipo umbali wa Kilometa 04 Kutoka makao makuu ya **Manispaa ya Musoma** na Kilomita 07 kutoka Stendi kuu ya Mabasi Bweri. Usafiri wa dalala kutoka mjini na stendi kuu ya mabasi Nauli ni Shilingi 500/=, kwa pikipiki Shilingi 2,000/= na kwa bajaji Shilingi 1,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/01/2026** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/01/2025 Mwisho wa kuripoti ni tarehe **27/01/2026.** Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili.**

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i. Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa kinachotolewa na Serikali (copy of Birth Certificate).
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. Kivuli cha matokeo ya elimu ya Msingi kama kipo

**Picha nne (04) “Passport Size” za Mwanafunzi na Picha moja moja “Passport Size” za Wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kusaidia katika malezi yake awapo shuleni.**

Ndugu Mzazi/Mlezi, Shule hii haina utaratibu wa chakula maalum (Special diet) kwa mwanafunzi mmoja mmoja tofauti na kile kinachoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wote. Vile vile shule ina mihula miwili (02) ya masomo na kila muhula unapokwisha shule huwa inafungwa. **Hivyo mzazi unatakiwa kumtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko. Shule hairuhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo.**

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha kamili ya vifaa vya lazima mwanafunzi anavyopaswa kuja navyo na fomu mbili anazotakiwa kujaza na kuja nazo wakati wa kuripoti shuleni.

Magita Gabriel Nyangore

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA**

**ORODHA KAMILI YA MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**

**SARE YA SHULE.**

Sare ya shule hii ni;

i. Mashati mawili mikono mifupi yanapatiakan
ii. Suruali mbili zenye **RANGI NYEUSI** mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma kulia **zisizobana na zisiwe "MODO (zinapatiakana karibu na shule kwa wataohitaji )**
iii. Suruali mbili za rangi ya damu ya Mzee – huvaliwa jioni baada ya saa za masomo (Zinapatikana karibu na Shule kwa atayehitaji)
iv. Overall (Ovalori) lenye mikono mifupi au mirefu lisilobana kwa ajili ya kuvaa wakati wa masomo ya ufundi kwa vitendo zinapatikana Shuleni.
v. 'T-SHIRTS' mbili za rangi ya NJANO zenye kola NYEUSI na michirizi ya Njano na vishikizo vitatu, zisizo na maandishi yoyote. Huvaliwa jioni baada ya saa za masomo zinapatikana shuleni zikiwa na mihuri kwa wataohitaji.
vi. Sweta la rangi ya kijani (kijani ya Mimea) lenye mshono au shingo ya **"V" na mstari mweupe .**
vii. Soksi jozi 2 za rangi nyeusi.
viii. Tai mbili (02) za rangi nyeusi na mistari myeupe zinapatikana karibu na Shule.
ix. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
x. Aje na viatu na nguo za michezo (Track Suit) ya rangi ya "Light Blue" kwa Kidato cha Kwanza.
xi. Pia aje n**a Jumping Rope – 01** kwa ajili ya michez**o.**
xii. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi au ugolo wa ukubwa wa kati usio na "bicross" kubwa.
xiii. Aje na Picha nne (PASSPORT SIZE) zilizopigwa akiwa na sare ya Shule kwa ajili ya Usajili (Awe na picha za wazazi walezi –kama kuna mzazi au mlezi wa maeneo ya karibu apewe kipaumbele kwa kuandikwa taarifa zake kwenye fomu na picha yake ili iwe rahisi kumfikia akihitajika.

**NB. Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuwa na nguo tofauti na hizo zilizo tajwa hapo juu. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa shuleni hapa.Akifika akapewa sare hatakiwi kabisa kuwa nguo za nyumbani)**

**VIFAA VYAKE BINAFSI VYA KUTUMIA BWENINI**

1. Aje na Godoro la "Sponge" la **2.5ft x 6 x 6**- zingatia vipimo tafadhali" (**Kama hataweza Godoro hili linapatikana karibu na shule kwa gharama ya Sh. 65,000/= ).**
2. Shuka mbili mpya rangi moja ya bluu bahari (Light blue)
3. Blanket
4. Mto na foronya
5. Chandarua
6. Ndala/Kandambili
7. Taulo
8. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake ni (lazima)
9. Ndoo moja ya kuchotea maji na dumu la lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji yake ya kunywa (Lazima).
10. Mwanafunzi aje na Toilet paper walau 10 kwa matumizi yake.
11. Sahani, bakuli, Kijiko na Kikombe cha nusu lita .

12. Kama mwanao ana tatizo la kukojoa kitandani ni lazima aje na godoro lililoshonewa cover la mpira wa kuzuia kupitisha mkojo.


13. **BIMA YA AFYA YA NHIF 50,400**

14. **VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Mathematical set
2. Kamusi (English Dictionary)
3. Madaftari makubwa (Counter Books) yasiyopungua 10.
4. Rim ya A3 moja yenye Karatasi za kuchorea (Hizi ni badala ya Daftari katika somo la Michoro).
5. Compass Set, Penseli za kuchorea na Set Square mbili za 30° / 60° na 45° kwa ajili ya Masomo ya Ufundi (Angalia kiambatatisho chenye picha). Zinapatikana kwenye maduka ya vifaa vya shule.


**Compass set. (VIFAA HIVI VINAPATIKANA KARIBU NA SHULE)**






Aina za Penseli (Nunua moja kwa kila fungu i – iii) .

(i) B-2-5............ Soft pencils
(ii) B, HB, H, F...... Medium soft /hard
(iii) 2H, 3H, 4H… Hard pencil



**SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

1. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
2. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na asubuhi ( Night & Monirning Preparation);
3. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
5. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
8. Kutunza mali za shule;
9. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
10. Mwanafunzi **haruhusiwi kubadili dini** wala kumshawishi mwanafunzi **mwenzake kubadili dini** wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani ila kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa tu**).

- **Musoma Sekondari ni Shule ya Mkondo wa Amali ambapo fani zifuatazo hutolewa; Electrical Installation, Refredration and Air Condition, capernty ,Welding and Metal Fabrication pamoja na Auto Electric. Tafadhali msaidie mwanao kuchagua fani moja wapo(Uchaguzi wa fani huendana na uhitaji na uwezo wa wkati huo. Ukihitaji ufafanuzi zaidi tuwasiliane kupitia namba zilizo tajwa hapo juu.**

- **Ukihitaji kumununulia Mwanao vitabu tafadhali nunua vitabu vya masomo haya yafuatayo ya AMALI; Historia ya Tanzania,Life skills,English Language, Mathematics, Computer Application, Technical Drawing , Engineering Science na Kitabu cha Fani yake.**

- **Mnamo Tarehe 10.02.2025 kutakuwa na kikao cha wazazi wa kidato cha kwanza tafadhali Fika bila kukosa kuanzi a saa tatu asubuhi.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xvii. Kucheza michezo ya kihuni kama betting,Games(**Play station**) na mingine kama hiyo.

***Zingatia: mwanafunzi atakayepatikana na simu shuleni atafukuzwa shule mara moja na kulipa faini ya tsh.200, 000/=.***
***Pia shule yetu kwa sasa imefanyiwa ukarabati mkubwa na serikali.hivyo mwanafunzi akijihusisha na uharibifu wa mali ya umma ikiwemo kuchafua kuta kwa maandishi,kuvunja taa,vioo,milango n.k atalazimika kufidia gharama za uharibifu huo.***

KARIBU SANA MUSOMA UFUNDI

**MAWASILINO: 0755671818 MKUU WA SHULE / 0767 082905 (M/Mkuu wa Shule)**

**A. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:**

1. Wizi.
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
3. Uvutaji bangi.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya/ Miadarati.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
8. Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
9. Kuoa/Kuolewa.
10. Kusababisha mimba.
11. Kusaidia kutoa mimba.
12. Kugoma, Kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani, usalama wa watu na mali ya umma.

13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoingia katika vipindi/ darasani au kukataa kufanya mtihani na mazoezi.
15. **Mwanafunzi kumiliki au kutumia au kukutwa na simu au "line" katika mazingira ya Shule.**

**ZINGATIA: MWANAFUNZI AKIKUTWA,KUTUMIA AU KUWA NA KIFAA CHA SIMU ATALIPA GHARAMA ZA UHARIBIFU WA MIUNDO MBINU NA ATAFUKUKULIWA HATUA ZAKINIDHAMU.**

**MWANAFUNZI AKIHARIBU MALI YA SHULE AU MIUNDO MBINU PAMOJA NA KUFUKUZWA SHULE NI LAZIMA ATALIPA GHARAMA ZA UHARIBIFU ALIO UFANYA**

FOMU: **NAMBA**

**1**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI KATIKA KIDATO CHA -------------------**

**MWAKA --------------------**

***(Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi pamoja na Mwanafunzi)***

Fomu hii ijazwe na mzazi/Mlezi pamoja na Mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia/Kuhamia kidato cha ---------------------------------------- kisha mwanafunzi ailete shuleni (**Ithibitishwe na Mwenyekiti/Mjumbe wa Kijiji/eneo unaloishi**)

1. Mimi------------------------------------------------(Jina la mwanafunzi) kwa hiari yangu, ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidato cha ------------------------ katika Shule ya Sekondari Musoma. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria zote za shule wakati wote niwapo shuleni. Kuvunja sheria ya shule kwa makusudi itakuwa nimekiuka ahadi hii ninayotoa na nitastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili hata kufukuzwa shule.

-----------------------------------

(Sahihi ya Mwanafunzi)
Tarehe ..............................

2. Mimi.................................................................(Jina la Mzazi/Mlezi) wa ............................................ ----------------------------

   Nakubali/sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni analazimika kufuata sheria za shule na kuwa mtiifu kwa walezi wake.Pia nakubali/sikubali kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

-----------------------------------

(Sahihi ya Mzazi/Mlezi)
Namba ya simu..................................

Tarehe ..............................

3. Mimi--------------------------------------- (Jina la mwenyekiti wa mtaa) ninathibitisha kuwa Ndugu------------------------------ ni Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa

   kuingia Kidato cha KWANZA ni mkazi wa kata ya ----------------------------------------------.

4. Namba ya simu ya Mwenyekiti (i).................................................................................

   Jina la MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI.................................................................................

   SAINI..................................................................TAREHE.....................................................

**FOMU: NAMBA 2**

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA NA KUKUBALI NAFASI**

Mimi.......................................................................................................-....................(jina kamili)

Kidato cha...........................................................................mwaka ..........................................................

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafuni na naahidi:-

(a) Kwamba nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya mamoniter, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.

(b) Kwamba nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(c) Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo na usio wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.

(d) Sitagoma wala kusababisha mgomo shuleni.

(e) Kwamba kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

Tarehe ............................................................. ----------------------------------------
Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe ............................................................. ----------------------------------------
Jina na Sahihi ya Shahidi Mzazi/Mlezi

Tarehe ............................................................. ----------------------------------------
Sahihi ya Mkuu wa Shule

**SHULE YA SEKONDARI MUSOMA FOMU YA**

**KUJIANDIKISHA SHULENI HABARI ZA**

**MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (Kama lilivyo kwenye TSM 9) ---------------------------------------------------
2. Tarehe ya kuzaliwa.................................................... Dini ...................................................
3. Mahali na Wilaya ulipozaliwa ...............................................................................................
4. Kata anayoishi kwa sasa.........................................................................................................
5. Shule ulipomaliza,Kidato ...........................................................................
6. Kidato unachokuja kuingia hapa shuleni ----------------------------------------------
7. Majina ya vyama vya masomo uliyowahi kujiunga:

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................
   (iii) ........................................................................---------------------------------------

8. Michezo/Masomo unayopendelea:

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................-------
   (iii) ..........................................................................................................

9. Kazi yeyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.

| **Madaraka/Uongozi** | **Shule/Mahali** | **Mwaka** |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

9. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (k.m. m ichezo, ushonaji n.k.)

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................
   (iii) ..........................................................................................................

Tarehe:.................................... ----------------------------------------------

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

## SHULE YA SEKONDARI MUSOMA UFUNDI

## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

### HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Baba ..................................................................................................
2. Kazi yake ..................................................................................................
3. Jina kamili la Mama ..................................................................................................
4. Kazi yake ...............................------..............................................................
5. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)
   ----------------------------------------------------------------------------------------------------------
6. Kazi na Anwani ya Mlezi ..................................................................................................
   ----------------------------------------------------------------------------------------------------------
7. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) ----------------------------------------------
   Kijiji/Mtaa..........................................................Wilaya..........................................................
   Kata..........................................................Mkoa..........................................................
   Tarafa ..........................................................
8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba ..................................................................................
   ----------------------------------------------------------------------------------------------------------

   Nambari ya simu..................................................................................-
9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama --------------------------------------------------------
   Nambari ya simu ..................................................................................................
10. Mtoto anaishi na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote
    (iv) Walezi **Kata isiyohusika***
11. Dini ya Baba..........................................................Dhehebu ..........................................................
    Dini ya Mama..........................................................Dhehebu ..........................................................
    Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ..........................................................
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa nakwenda siku za likizo: --
    ----------------------------------------------------------------------------------------------------------
13. Mimi..........................................................(Baba/Mama/Mlezi wa ..........................................................
    ..........................................................Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na haahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe..........................................................
.

..........................................................
Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi

BANDIKA PICHA ZA WAZAZI/WALEZI HAPA CHINI KISHA ANDIKA UHUSIANO CHINI YA PICHA

FOMU: NAMBA 5

# MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in Government Hospital in respect of all new entrants to Musoma Secondary School.

Full Name: ........................................................................................................................................

Age: ...................................................................................................................................................

1. Chest : ..........................................................................................................................
2. Blood count (Red and White) ..........................................................................................
3. Urine Examination ..........................................................................................................
4. Stool Examination ..........................................................................................................
5. Syphilis Test ..................................................................................................................
6. T.B. Test ........................................................................................................
7. Ear Test ........................................................................................................
8. Eye Test ........................................................................................................
9. Spleen ...........................................................................................................
10. Abdomen ........................................................................................................
11. Addition information of any other physical, mental hereditary of infectious diseases:

---------------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------------

Treatment after examination ..............................................................................................

---------------------------------------------------------------------------------------------------------

**(Please state nature of treatment)**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature ..................................................................

Designation..................................................................

Station: ..................................................................

Date.........................................................

Official Stamp